**SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR**
**WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA AMALI**

# FURSA MBALIMBALI ZA UFADHILI WA MASOMO NA TAFITI NCHINI JAPAN.

Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, Zanzibar Inapenda kutoa taarifa kuhusu uwepo wa fursa mbalimbali za ufadhili wa masomo na tafiti nchini Japan, zinazotolewa na wadau mbalimbali wa maendeleo. Fursa hizo zinajumuisha ufadhili unaotolewa na:

i. Serikali ya Japan kupitia Wizara ya Elimu, Utamaduni, Michezo, Sayansi na TeknoLojia (MEXT Scholarship);
ii. Shirika la Kimataifa la Maendeleo la Japan (JICA) — programu za JICA hutoa mafunzo ya muda mfupi na muda mrefu kwa watumishi wa umma, wataalamu, wanasayansi na viongozi wa taasisi mbalimbali kutoka Tanzania;
iii. Mashirika binafsi ya Kijapani yanayotoa ufadhili wa kujitegemea kwa wanafunzi wa kimataifa; na
iv. Vyuo vikuu vinavyotoa ufadhili moja kwa moja kupitia University-Specific Scholarships kwa wanafunzi wa kimataifa.

Aidha, sehemu kubwa ya ufadhili huu ni kwa ngazi ya Uzamili (Master's) na Uzamivu (PhD). Wizara ya Elimu ya Japan (MEXT) pia hutoa ufadhili kwa ngazi ya Shahada ya Kwanza (Undergraduate) na Masomo ya Ufundi (Specialized Training).

Taarifa zaidi kuhusu fursa hizi, zikiwemo sifa za waombaji na taratibu za maombi, zinapatikana kupitia tovuti za kila taasisi husika ambazo zimeambatishwa.

Vilevile, taarifa za scholarships zinazopatikana Japan, ambapo baadhi zimekuwa zikitolewa kwa Watanzania, zinapatikana kupitia kiunganishi (link) ifuatayo:
STUDY IN JAPAN-Scholarship Pamphiet:
https://www.studyinjapan.go.ip/en/planning/brochures/#002

Tunashauri Watanzania wenye nia ya kusoma au kufanya tafiti nchini Japan kutembelea tovuti hii mara kwa mara ili kubaini fursa mpya zinapowekwa kwa mwaka husika wa masomo.

Imetolewa na;

Katibu Mkuu,
Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali,
S.L.P. 394,
ZANZIBAR. -
***Email:*** **unt.hest@moez.go.tz | hestpemba@moez.go.tz**